# SHERIA YA KUANZISHA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR, KUWEKA MASHARTI YA UONGOZI, UDAHILI, PROGRAMU ZA MAFUNZO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU MAELEZO

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.

### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

3. Kuanzishwa kwa Skuli.

4. Kazi na uwezo wa Skuli.

### SEHEMU YA TATU
### UTAWALA

5. Baraza la Skuli.

6. Sifa za Mwenyekiti.

7. Uwezo na kazi za Baraza.

8. Misingi ya uongozaji wa Skuli.

9. Muda wa kutumikia nafasi.

10. Nafasi ya Mwenyekiti au mjumbe kuwa wazi.

11. Vikao vya Baraza.

12. Akidi na maamuzi.

13. Kumbukumbu za vikao kurekodiwa.

14. Posho za wajumbe wa Baraza.

15. Kamati na kukasimu.

16. Mkuu wa Skuli.

17. Naibu Wakuu wa Skuli.

18. Wafanyakazi.

**SEHEMU YA NNE**
**UDAHILI NA PROGRAMU ZA MAFUNZO**

19. Masharti ya Udahili.

20. Maombi ya kudahiliwa.

21. Programu za Masomo.

22. Vigezo vya tathmini na vyeti vya taaluma.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA FEDHA**

23. Fedha za Skuli.

24. Matumizi ya fedha.

25. Makadirio ya mwaka.

26. Hesabu na ukaguzi.

**SEHEMU YA SITA**
**MASHARTI MENGINEYO**

27. Kinga dhidi ya dhima binafsi.

28. Dhima ya Baraza kwa hasara itakavyojitokeza.

29. Makosa na Adhabu.

30. Kanuni.

**SHERIA NAM. 13 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

30 Disemba ..........................................................., **2019**

# SHERIA YA KUANZISHA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR, KUWEKA MASHARTI YA UONGOZI, UDAHILI, PROGRAMU ZA MAFUNZO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Skuli ya Sheria Zanzibar, 2019 na itaanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vyenginevyo:

"Baraza" maana yake ni Baraza la Skuli lililoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya sheria;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Mkuu wa Skuli" maana yake ni Mkuu wa Skuli aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 16 cha Sheria hii;

"Wakili au vakili mwenye sifa" maana yake ni Wakili au vakili anayetambuliwa na sheria inayohusiana na mawakili;

"Skuli" maana yake ni Skuli ya Sheria Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii; na

"Mwanafunzi" maana yake ni mtu aliyedahiliwa kwa ajili ya mafunzo yoyote yanayoendeshwa na Skuli.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA SKULI YA SHERIA ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Skuli.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Skuli itakayojulikana kama Skuli ya Sheria Zanzibar ambayo itakuwa ni chombo chenye kujitegemea, chenye urithi wa kuendelea na chenye muhuri wake na kwa jina lake, kinaweza:

(a) kushtaki au kushtakiwa;

(b) kuingia katika mikataba;

(c) kuchukua, kununua, au vyenginevyo kujipatia, kumiliki, kuendeleza au kuondosha mali inayohamishika au isiyohamishika;

(d) kukopa au kuchangisha fedha;

(e) kuwekeza na kutunza fedha za Skuli ambazo hazihitajiki kwa matumizi ya haraka, katika utaratibu utakaowekwa na Skuli kila baada ya muda; na

(f) kufanya au kutekeleza mambo mengine yoyote au vitendo ambavyo kisheria vinaweza kufanywa na chombo kinachojitegemea.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Skuli kwa waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkuu wa Skuli au Naibu Mkuu wa Skuli aliyeidhinishwa na Mkuu wa Skuli.

(3) Waraka wowote ili uwe ni hati halali iliyotolewa na Skuli, utatakiwa kuwekwa muhuri wa Skuli na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi na uwezo wa Skuli.

**4.**-(1) Kazi za Skuli zitakuwa ni:

(a) kuwafunza watu wapate kuwa mawakili au vakili wenye sifa;

(b) kuwapatia mafunzo endelevu ya ukuzaji taaluma kwa aina zote za wataalamu wa sheria;

(c) kutoa mafunzo kwa wasaidizi wa sheria kwa kushauriana na Idara ya Msaada wa Kisheria iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Msaada wa Kisheria;

(d) kutoa mafunzo mengine maalumu katika sekta za sheria;

(e) kuandaa mitaala, miongozo ya mafunzo na kuendesha mitihani yenye ubora pamoja na kutunuku vyeti vya taaluma;

(f) kuanzisha miradi, tafiti na kutoa ushauri elekezi; na

(g) kushughulikia uchapishaji na usambazaji wa tafiti za kisheria zinazotokana na kazi za Skuli kama itakavyoamuliwa na Baraza.

(2) Skuli inaweza kuanzisha mahusiano au mashirikiano na vyuo na taasisi nyengine kitaifa na kimataifa.

## SEHEMU YA TATU
## UTAWALA

Baraza la Skuli.

**5.**-(1) Kutakuwa na Baraza la Skuli ambalo litajumuisha:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkuu wa Skuli ambaye atakuwa ni mjumbe kwa nafasi yake;

(c) Jaji mmoja wa Mahakama Kuu ya Zanzibar;

(d) Mwanachama hai mmoja kutoka Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar;

(e) Wakili wa Serikali mmoja kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(f) Mjumbe mmoja kutoka taasisi ya elimu ya juu; na

(g) Mjumbe mmoja kutoka Idara ya Msaada wa Kisheria.

(2) Wajumbe wote chini ya aya (c), (d), (e), (f) na (g) za kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri baada ya kushauriana na taasisi zao husika.

(3) Naibu Mkuu wa Skuli anayehusika na taaluma atakuwa Katibu wa Baraza.

Sifa za Mwenyekiti.

**6.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, iwapo mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana shahada katika fani yoyote inayotambulika;

(c) ana uzoefu katika fani hiyo usiopungua miaka saba; na

(d) anaheshimika katika jamii.

Uwezo na kazi za Baraza.

**7.**-(1) Baraza kwa kuzingatia Sheria hii, litakuwa na jukumu la usimamizi na uongozi wa jumla wa Skuli na litatoa maelekezo katika mambo yanayohusu Skuli.

(2) Bila ya kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza litafanya kazi zifuatazo:

(a) litatoa miongozo katika utayarishaji wa:

(i) mipango mikakati ya maendeleo;

(ii) programu za mafunzo; na

(iii) programu za kujenga uwezo.

(b) litaidhinisha mitaala na programu za mafunzo;

(c) litaidhinisha ada za mafunzo na malipo zinazotokana na huduma mbalimbali zinazotolewa na Skuli;

(d) litaidhinisha ratiba za mitihani;

(e) litathibitisha matokeo ya mtihani.

(f) litasimamia na kutathmini utendaji wa Skuli;

(g) litasimamia mali na fedha za Skuli kwa uwazi na uwajibikaji na kwa madhumuni ya kuendeleza kazi za Skuli;

(h) litaajiri maofisa na wafanyakazi wa Skuli kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma; na

(i) litaidhinisha na kuwasilisha kwa Waziri makisio ya bajeti inayohusiana na Skuli.

(3) Baraza litakuwa na uwezo wa :

(a) kufanya maamuzi ya kisera ambayo yataimarisha utendaji wa Skuli;na

(b) kuandaa kanuni ambazo zitaonekana ni za lazima katika utaratibu wa usimamizi wa masuala ya Skuli zinazoelezea:

(i) vigezo vya tathimini kwa ajili ya utoaji wa vyeti vya taaluma;

(ii) aina ya mitihani na namna ya uendeshaji wa mitihani;

(iii) uanzishaji na usimamizi wa kituo cha utafiti na mafunzo katika elimu ya sheria kwa ajili ya kufikia malengo ya Skuli;

(iv) viwango vya ada na malipo mengine kwa huduma zitakazotolewa na Skuli;

(v) usimamizi na nidhamu ya wanafunzi wa Skuli;

(vi) Kanuni za Maadili kwa wanafunzi na wafanyakazi wa Skuli; na

(vii) mashirikiano na taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya Zanzibar ambazo zina malengo yanayofanana na yale ya Skuli.

(c) kufanya kazi nyengine kama itakavyopewa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote.

(4) Baraza litakuwa pia na wajibu wa kuaandaa muundo wa utumishi na muundo wa Skuli kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma .

Misingi ya uongozaji wa Skuli.

**8.** Katika kutekeleza kazi zake na kutumia uwezo wake chini ya Sheria hii, Skuli itazingatia misingi ifuatayo:

(a) kudumisha maadili na taaluma;

(b) kufikia ubora wa kiwango cha juu;

(c) kutokubagua; na

(d) uwajibikaji.

Muda wa kutumikia nafasi.

**9.**-(1) Mwenyekiti wa Baraza atashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne lakini anaweza kuteuliwa tena.

(2) Mjumbe wa Baraza atashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena.

Nafasi ya Mwenyekiti au Mjumbe kuwa wazi.

**10.**-(1) Nafasi ya Mwenyekiti au mjumbe wa Baraza itakuwa wazi ikiwa Mwenyekiti au mjumbe huyo:

(a) atajiuzulu nafasi yake kwa taarifa ya maandishi atakayoipeleka kwa mamlaka ya uteuzi;

(b) hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza bila ya ruhusa ya Mwenyekiti;

(c) ametiwa hatiani na Mahakama kwa kosa na ameadhibiwa kutumikia kifungo kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita;

(d) ametiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na udanganyifu, kukosa uaminifu au kukosa maadili;

(e) hawezi, kutekeleza kazi zake kama mjumbe wa Baraza kutokana na maradhi ya akili au mwili;

(f) ametamkwa na Mahakama kuwa amefilisika;

(g) vyenginevyo hana uwezo au hana sifa za kuendelea kuwa mjumbe wa Baraza; au

(h) amefariki.

(2) Endapo mjumbe yeyote wa Baraza amesita kuwa mjumbe kwa sababu yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mamlaka ya uteuzi inaweza kumteua mjumbe mwengine kushika nafasi ya mjumbe huyo, na mjumbe aliyeteuliwa atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki cha mjumbe aliyetangulia.

Vikao vya Baraza.

**11.**-(1) Baraza litakaa vikao vyake katika muda na pahala ndani ya Zanzibar kama litakavyoona inafaa lakini litakaa mara moja katika kila miezi mitatu.

(2) Kikao chochote cha Baraza, kisichokuwa kikao cha kawaida, kitajulikana kama kikao cha dharura na kinaweza kuitishwa wakati wowote Mwenyekiti atakapoona inafaa.

(3) Taarifa ya wakati, pahala na ajenda za kila kikao cha Baraza zitatolewa na katibu kwa kila mjumbe wa Baraza.

(4) Kwa kikao cha kawaida, taarifa itatolewa kwa kila mjumbe si chini ya siku kumi na nne kabla ya kikao, na kwa kikao cha dharura, si chini ya saa arubaini na nane kabla ya kikao.

Akidi na maamuzi.

**12.**-(1) Akidi ya vikao vya Baraza itakuwa angalau zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Baraza.

(2) Maamuzi yote ya Baraza yatafanywa kwa makubaliano ya pamoja.

(3) Na iwapo pameshindikana makubaliano ya pamoja, maamuzi yatafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe waliohudhuria.

(4) Itakapotokea kura kuwa sawa Mwenyekiti atakuwa na kura ya kawaida na kura ya maamuzi.

(5) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Baraza ambacho anahudhuria, na akiwa Mwenyekiti hayupo katika kikao, wajumbe waliohudhuria watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuongoza kikao na atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti.

(6) Baraza linaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chochote cha Baraza iwapo linaona kuwa elimu na uzoefu wake utasaidia Baraza, na atashiriki katika majadiliano lakini hatakuwa na kura.

Kumbukumbu za vikao kurekodiwa.

**13.** Baraza litawezesha kuchukuliwa na kurekodiwa kumbukumbu sahihi za vikao vyote vya Baraza.

Posho za wajumbe wa Baraza.

**14.** Wajumbe wa Baraza watalipwa posho kama Waziri atakavyoidhinisha kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Kamati na kukasimu.

**15.**-(1) Baraza linaweza kuanzisha Kamati miongoni mwa wajumbe kama litakavyoona inafaa.

(2) Baraza linaweza, kwa azimio, ama kwa ujumla au kwa jambo maalum, kukasimu kwa Kamati yoyote au mjumbe yeyote, ofisa, mfanyakazi au wakala wa Baraza, utekelezaji wa kazi yoyote ya Baraza chini ya Sheria hii.

Mkuu wa Skuli.

**16.**-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Skuli ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkuu wa Skuli aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Skuli.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Skuli endapo mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya Sheria na uzoefu usiopungua miaka saba katika fani hiyo; na

(c) ana kiwango cha juu cha maadili na tabia njema.

(4) Mkuu wa Skuli, kwa maelekezo ya Baraza atakuwa na wajibu wa usimamizi wa kazi za kila siku za Skuli.

(5) Bila ya kujali masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki, Mkuu wa Skuli atakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakikisha anaendeleza ufanisi na nidhamu kwa wafanyakazi wote wa Skuli;

(b) kuendesha mitihani kwa mujibu wa ratiba iliyoidhinishwa na Baraza;

(c) kusimamia bajeti ya Skuli kwa kuhakikisha kwamba fedha zake zinatumika kwa usahihi na kudhibitiwa; na

(d) kutekeleza majukumu mengine kama atakavyoagizwa na Baraza kila baada ya muda.

(6) Mkuu wa Skuli atashika nafasi yake kwa kipindi cha miaka minne na anaweza kuteuliwa tena.

Naibu Wakuu wa Skuli.

**17.**-(1) Kutakuwa na Naibu Wakuu wawili wa Skuli mmoja anayehusika na taaluma na mwengine anayehusika na utawala ambao watateuliwa na Rais.

(2) Sifa za Naibu Wakuu wa Skuli zitakuwa ni angalau shahada ya kwanza ya sheria, utawala, uchumi au fani nyengine inayofanana na hizo.

(3) Naibu Wakuu wa Skuli watashikilia nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena.

(4) Naibu Wakuu wa Skuli watateuliwa kupitia utaratibu wa uajiri wa ushindani kwa vigezo na masharti ya ajira kama Rais atakavyoamua.

(5) Naibu Mkuu wa Skuli anayehusika na Taaluma atakuwa msaidizi wa karibu, na atawajibika kwa Mkuu wa Skuli katika masuala yote yanayohusiana na shughuli za taaluma za Skuli.

(6) Naibu Mkuu wa Skuli anayehusika na utawala atakuwa msaidizi wa karibu, na atawajibika kwa Mkuu wa Skuli katika masuala yote yanayohusiana na shughuli za utawala wa Skuli.

Wafanya kazi.

**18.** Baraza litaajiri maofisa na wafanyakazi wa Skuli kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi za Skuli kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

## SEHEMU YA NNE
## UDAHILI NA PROGRAMU ZA MAFUNZO

Masharti ya Udahili.

**19.** Mtu hatakuwa na sifa ya kudahiliwa kwa masomo ya Skuli, isipokuwa mtu huyo awe ametimiza masharti ya udahili kama yatakavyoainishwa katika Kanuni.

Maombi ya kudahiliwa.

**20.**-(1) Mtu ambaye anataka kudahiliwa katika masomo yoyote ya Skuli ataomba kwa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni.

(2) Skuli itazingatia maombi yaliyowasilishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, na iwapo itaridhika kuwa muombaji ametimiza masharti ya udahili, itamdahili muombaji katika Skuli.

Programu za Masomo.

**21**. Baraza litaamua na kuchapisha katika Kitabu cha Skuli cha Programu za Masomo:

(a) programu za taaluma na masomo; na

(b) kalenda ya taaluma, ikijumuisha muda wa masomo kwa kila fani.

Vigezo vya tathmimi na vyeti vya taaluma.

**22.**-(1) Skuli itamtathmini mwanafunzi kwa kila somo, kwa kutumia vigezo vilivyoelezwa katika Kanuni.

(2) Endapo Skuli itaridhika na vigezo vya kutathimini chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza linaweza kutoa cheti, stashahada au stashahada ya uzamili.

(3) Baraza linaweza kukifuta na kukichukua cheti iwapo cheti hicho kitagundulika kuwa kimepatikana kwa njia ya udanganyifu.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Skuli.

**23.** Fedha za Skuli zitatokana na:

(a) fedha zitakazoweza kuidhinishwa kama ruzuku na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zote zitakazolipwa Skuli kwa njia za ada, msaada, michango, wasia, zawadi, malipo, kodi ya pango au riba;

(c) fedha zote zitakazokopwa kwa madhumuni ya Skuli kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) fedha zozote au mali ambazo zinaweza kulipwa au kupewa Skuli kuhusiana na utekelezaji wa kazi zake.

Matumizi ya fedha.

**24.** Fedha za Skuli zitatumika kwa:

(a) gharama zilizoingiwa na Skuli katika kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii;

(b) malipo ya mishahara, posho, na malipo mengine yanayohusiana na wafanyakazi wa Skuli;

(c) uwekezaji wa fedha ambazo ni sehemu ya fedha za Skuli na hazihitajiki kutumiwa kwa wakati huo kwa madhumuni yoyote;

(d) malipo ya fedha zozote zilizokopwa na Skuli na malipo ya riba kwa fedha zozote zilizokopwa; na

(e) matumizi yote yaliyofanywa kuhusiana na uanzishaji, ununuzi wa vifaa au usimamizi wa Skuli.

Makadirio ya mwaka.

**25.**-(1) Angalau miezi sita kabla ya kuanza mwaka wa fedha, Baraza litawezesha kuandaliwa makadirio ya mapato na matumizi ya Skuli kwa mwaka huo wa fedha.

(2) Makadirio ya mwaka yataainisha vifungu vya makadirio yote ya matumizi ya Skuli kwa mwaka wa fedha husika, makadirio yataonesha:

(a) malipo ya mishahara, posho, na malipo mengine kuhusiana na wafanyakazi wa Skuli;

(b) matengenezo stahiki ya majengo na maeneo ya Skuli;

(c) matengenezo, marekebisho na kubadilisha vifaa na mali nyengine yoyote ya Skuli; na

(d) matumizi yote yatakayofanywa yanayohusiana na uanzishaji, vifaa au usimamizi wa Skuli.

(3) Makadirio ya mwaka yatazingatiwa na Baraza kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha unaohusu makadirio hayo na yatawasilishwa kwa Waziri kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(4) Matumizi hayatafanywa kwa madhumuni ya Skuli isipokuwa kwa mujibu wa makadirio ya mwaka yaliyoidhinishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki.

Hesabu na ukaguzi.

**26.**-(1) Baraza litawezesha kuwekwa kwa vitabu na kumbukumbu sahihi za mapato, matumizi na mali za Skuli.

(2) Hesabu za Skuli zitakaguliwa na kutolewa taarifa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Sheria ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Kinga dhidi ya dhima binafsi.

**27.** Hakuna jambo au kitu kitakachofanywa na mjumbe wa Baraza au ofisa yeyote, mfanyakazi au wakala wa Skuli kitakachomuwajibisha binafsi mjumbe, ofisa, mfanyakazi au wakala au mtu yeyote anayefanya kazi kwa maelekezo yake katika kesi, malalamiko au madai yoyote, endapo jambo hilo au kitu hicho kitafanywa kwa nia njema kwa ajili ya utekelezaji wa kazi, uwezo au jukumu la Skuli.

Dhima ya Baraza kwa hasara itakayojitokeza.

**28.** Masharti ya kifungu cha 27 cha Sheria hii hayataliepusha Baraza dhima ya kulipa fidia au hasara kwa mtu yeyote kwa madhara aliyoyapata, mali yake au sehemu ya maslahi yake yaliyosababishwa na utekelezaji wa mamlaka iliyopewa chini ya Sheria hii au kwa kushindwa kutekelea kazi zake zote au sehemu ya kazi zake.

Makosa na Adhabu.

**29.**-(1) Mtu ambaye kwa kujua, kwa madhumuni ya kupata udahili au usajili wake mwenyewe au mtu mwengine kama mwanafunzi wa Skuli, au kwa madhumuni mengine yoyote chini ya Sheria hii:

(a) anatoa maelezo ya uongo au taarifa; au

(b) anatoa au anawasilisha au anasababisha kutoa au kuwasilisha waraka wowote au taarifa ambayo ni ya uongo kiuhalisia,

anatenda kosa.

(2) Mtu ambaye anatenda kosa chini ya kifungu hiki atawajibika akitiwa hatiani kulipa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili.

Kanuni.

**30.** Waziri anaweza, kwa ujumla, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 5 Disemba, 2019.

..............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***